

Jina _____

Nambari ya mwanafunzi

Jinsia Mume Mke

Jina la kaunti _____ Nambari la kaunti

Jina la kaunti ndogo _____ Nambari la kaunti ndogo

Jina la shule _____ Nambari la shule

VIWANGO VYA KUTATHMINI

	Kuzidisha matarajio	Kufika matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
Sehemu ya 1				
Sehemu ya 2				
Sehemu ya 3				
Sehemu ya 4				

SEHEMU YA I

1. KUZUNGUMZA NA KUSIKILIZA

(a) Habari ya asubuhi?

(mwanafunzi kujibu)

(b) Mnasoma gredi la ngapi?

(mwanafunzi kujibu)

(ch) Mnapenda mchezo gani?

(mwanafunzi kujibu)

(d) Jina la mwalimu mkuu?

(mwanafunzi kujibu)

2. Senemu ya 2:

Kusoma

Alama za barabarani ni muhimu. Watu wanaendesha magari wanastahili kuzingatia alama hizo. Alama ya kivukio cha watoto huwekwa karibu na shule. Wanaotumia barabara wanafaa kuwa waangalifu wanapokiona. Ni hatari kwa watoto kucheza au kukimbizana barabarani. Alama nyingine ni herufi H inayoonyesha hospitali. Dereva anapofika hapo ni lazima awe mwangalifu na apunguze kasi ya gari lake vilevile, haruhusiwi kupiga honi ovyoovyoo karibu na shule au hospitali. Alama nyingine ni kivukio cha wanyama na kivukio cha watu. Alama na sheria za barabarani zinapofuatwa, ajali hupungua.

3. Sehemu ya 3:

Soma kifungu kisa ujibu maswali?

Shule yetu inaitwa Bonda ina madarasa manane na wanafunzi mia tano hamsini. Walimu wetu ni tisa. Walimu hawa hufanya kazi ya ualimu, yaani kufundisha wanafunzi. Mwalimu mkuu ni Bwana Juma Koyana. Yeye ndiye msimamizi mkuu wa shule. Bi Chebet ni naibu wa mwalimu mkuu. Yeye humsaidia mwalimu mkuu kusimamia shule haswa katika upande wa nidhamu. Bi Chebet. Pia ni mwalimu wa darasa letu. Yeye hapendi wanafunzi wanaorandaranda ovyo darasani.


Kiranja wa darasa letu anaitwa zafani mwongera. Yeye ni mwanafunzi mwenye bidii za mchwa na hufanya vyema darasani. Siku moja, wakati wa mvua hakuweza kubeba vitabu kumpelekea mwalimu.

1. Jibu maswali

- (a) Shule ya msimulizi inaitwa aje? _____
- (b) Jina la mwalimu mkuu ni _____
- (c) Naibu wa mwalimu mkuu anaitwa nani? _____
- (d) Shule hii ina madarasa mangapi? _____
- (e) Kiranja wa darasa la mwandishi ni _____
- (f) Kuna wanafunzi wa ngapi katika shule hii? _____
- (g) _____ ndiye ana shughulikia mambo ya nidhamu.

2. Tumia 'enyewe' kujaza pengo
mfano: Mfoto mwenyewe ni mgonjwa
(a) Mwalimu _____ alitupa kazi ya ziada.
(b) Kitanda _____ kilivunjika.
(c) Chungwa _____ ni chungu.

3. Chora picha (mpira juu ya meza)



SEHEMU YA 4

Andika insha kuhusu

RAFIKI YANGU
